PENTECOSTAL ASSEMBLIES OF GOD (TANZANIA)
HEAD OFFICE: P.O. BOX 3390 DODOMA, TANZANIA. Tel. 026-2350019

# MWONGOZO WA MAOMBI NA KUFUNGA KWA SIKU 21 KUANZIA TAREHE 8-28/01/2024

**Ni wakati wa mambo makubwa, Inuka uangaze. Yeremia 33:3**

KITABU CHA MPANGO MKAKATI SURA YA 4 UKURASA WA 35 KINAELEKEZA KUENDESHA MAOMBI YA SIKU 21 MARA MOJA KWA MWAKA. MAMBO YOTE YALIYOANDIKWA KWA KILA SIKU NDANI YA SIKU 21 YANAHITAJI MAOMBI YAKO.

| WIKI YA KWANZA: Januari 8 – 14, 2024 | | |
|---|---|---|
| **TAREHE** | **MAHITAJI YA KUOMBEA** | **MISTARI YA KUSIMAMIA** |
| **08/01/2024 JUMATATU** | **SHUKRANI.**<br>- Mshukuru Mungu kwa yote kwa mwaka mzima kuanzia Januari hadi Desemba, 2023. | 1 Mambo ya Nyakati 16:34.<br>1 Wathesalonike 5:18. |
| **09/01/2024 JUMANNE** | **TOBA NA KUJIWEKA WAKFU KWA MUNGU.**<br>- Tubu, kujitakasa na kuomba rehema za Mungu katika maisha yako na kwa ajili ya wengine.<br>- Roho Mtakatifu akuongoze kuomba sawasawa na mapenzi ya Mungu. | 2 Wakorintho 7:1.<br>Mathayo 3:8.<br>Warumi 8:26-27. |
| **10/01/2024 JUMATANO** | **HOFU YA MUNGU.**<br>- Mungu akupe roho ya kumwabudu yeye katika roho na kweli, maana Mungu hutafuta watu kama hao.<br>- Ibada zetu zijae nguvu za Roho Mtakatifu.<br>- Ishi maisha matakatifu ya kujitenga na dhambi daima. | Yohana 4:23-24.<br>1 Wakorintho 2:4.<br>Mathayo 11:12 |
| **11/01/2024. ALHAMISI** | **UCHAGUZI WA VIONGOZI 2024.**<br>- Mungu atupe viongozi wanaotoka kwake watakaolisimamia kusudi lake katika Kanisa letu la PAG Tanzania.<br>- Wapiga kura wote waongozwe na Roho Mtakatifu ili kupata viongozi bora kwa ngazi zote katika mwaka huu wa Uchaguzi.<br>- Uchaguzi wa Serikali za vijiji na mitaa ufanyike kwa amani na utulifu. | Matendo 1:24.<br>Warumi 8:14. |

| | | |
|---|---|---|
| **12/01/2024 IJUMAA** | **KUISHI KATIKA MAADILI MEMA.**<br>- Uwe kielelezo mbele ya jamii inayokuzunguka katika maneno na matendo maana wewe ni barua ya Kristo Yesu.<br>- Mungu akusaidie kutenda sawasawa na Maadili ya Msingi yaliyoko katika kitabu cha **Mpango mkakati wa PAG Tanzania wa miaka kumi 2021 hadi 2031 katika sura ya 3 ukurasa wa 8-10.** | 2 Wakorintho 3:2<br><br>1 Wakorintho 14:40 |
| **13/01/2024 JUMAMOSI** | **HUDUMA ZA JAMII.**<br>- Jitoe kikamilfu kumhudumia mwanadamu katika maswala ya kijamii huduma za elimu, afya, miundo mbinu nk.<br>- Mungu akuwezeshe kuwahudumia wahitaji kwa mfano wazee, wagonjwa, wafungwa, watoto yatima nk. | Matendo 6: 1-7<br><br>Luka 10:25-37 |
| **14/01/2024 JUMAPILI** | **HESHIMA.**<br>- Uwe na roho ya upendo na kuwaheshimu wenzako na kuwajali maana tumeumbwa kwa mfano wa Mungu.<br>- Tuwaheshimu viongozi wetu na kufuata maelekezo wanayotuelekeza na kuitendea kazi. | 1 Yohana 4:20-21.<br><br>1 Wathesalonike 4:2 |
| | | |

| WIKI YA PILI – Januari 15 – 21, 2024 | | |
|---|---|---|
| **TAREHE** | **MAHITAJI YA KUOMBEA** | **MISTARI YA KUSIMAMIA** |
| **15/01/2024 JUMATATU** | **UMOJA.**<br>- Kataa utengano wowote na kujiepusha na roho ya ugomvi, fitina, faraka, husuda na matukano. Maana watendao mambo kama hayo ni wale wenye tabia ya mwilini.<br>- Hamasisha umoja wa mwili wa Kristo kuanzia ngazi ya chini hadi juu katika kanisa la PAG Tanzania. Maana sisi zote tunategemeana tu viungo katika mwili kujenga kanisa imara.<br>- Mungu ameamuru baraka palipo na UMOJA.<br>- Mungu wa amani ashushe amani mashariki ya kati, taifa la Israeli na mataifa mengine duniani kote. | 1 Wakorintho 3:1-3.<br>1 Wakorintho 12:1-27.<br>Yohana 17:21.<br>Zaburi 133:3 |
| **16/01/2024 JUMANNE** | **UHARAKA.**<br>- Achana na roho ya ukawaida, na kufanya kazi kwa ulegevu kwa sababu roho hiyo hudhoofisha kazi ya Umisheni.<br>- Itikia maswala ya ngazi zote kwa haraka na kuchukua hatua stahiki katika utekelezaji wenye ufanisi. | Mathayo 28:18-20.<br>Yeremia 48:10.<br>Warumi 13:11. |
| **17/01/2024 JUMATANO** | **UWAKILI.**<br>- Jitambue wewe ni wakili wa Mungu hapa duniani vitu vyote ni vya Mungu yaani watu, fedha na muda, na | 1 Wakorintho 4:1-2.<br>Danieli 6:1-3<br>Mwanzo 2:15. 39:4. |

| | | |
|---|---|---|
| | umekabidhiwa kwa ajili ya kujenga Ufalme wa Mungu.<br>- Kinachohitajika ni kuwa mwaminifu katika kuendeleza rasilimali hizo. | |
| **18/01/2024 ALHAMISI** | **UWAZI NA UWAJIBIKAJI.**<br>- Fuata na kutii kanuni, taratibu na miongozo tuliyojiwekea wenyewe kwa uadilifu bila udanganyifu. Mungu wetu ni Mungu wa utaratibu<br>- Tumia falsafa ya kutovumilia ubadhilifu wowote wa rasilimali ya Mungu tuliyokabidhiwa na tuwajibishane katika mifumo tuliyojiwekea. | 1 Wakorintho 14:40.<br><br>Yakobo 5:19-20. |
| **19/01/2024 IJUMAA** | **MABADILIKO.**<br>- Uwe na roho ya kupokea mabadiliko kwa moyo wa upendo wewe binafsi katika fukra zako na kanisa lote kwa ujumla. Mungu muumba wa mbingu na nchi na vilivyomo ni Mungu wa Mabadiliko.<br>- Binadamu hupitia katika mabadiliko ya moyo, mifumo na miundo. Kwa kuwa ni Wakati wa Mambo Makubwa utegemee mabadiliko ya utendaji.<br>**Mpango Mkakati ukurasa wa 10.** | Mathayo 5:17.<br><br>Warumi 12:2<br><br>Yeremia 33:3. |
| **20/01/2024 JUMAMOSI** | **UMISHENI.**<br>- Tii agizo kuu la Bwana wetu Yesu Kristo.<br>- Omba Mungu atume watenda kazi katika shamba lake, maana watenda kazi ni wachache. | Mathayo 28:18-20.<br>Luka 10:2.<br>Hagai 2:8.<br>Warumi 10:15. |

| | | |
|---|---|---|
| | - Idara ya Umisheni na Uinjilisti ipate rasilimali watu na fedha ili kutimiza agizo kuu.<br>**Mpango mkakati ukurasa wa 46.** | |
| **21/01/2024 JUMAPILI** | **ELIMU NA MAFUNZO.**<br>- Uwe na moyo wa kujiendeleza kielimu maana ngazi uliyofikia siyo mwisho wa elimu na maarifa.<br>- Neema ya Mungu iwe juu ya wakurugenzi wote wa idara hiyo katika ngazi zote na waalimu wote wanaofundisha katika vyuo na shule zote.<br>**Mpango mkakati Ukurasa wa 61.** | Mithali 4:13.<br><br>1 Wakorintho 3:10. |
| | | |

## WIKI YA TATU – Januari 22-28, 2024

| TAREHE | MAHITAJI YA KUOMBEA | MISTARI YA KUSIMAMIA |
|---|---|---|
| **22/01/2024 JUMATATU** | **WASHIRIKA WENZA.**<br>- Mungu afungue mlango wa washirika wenza walio sahihi kushirikiana na PAG Tanzania katika kuujenga Ufalme wa Mungu.<br>- Kazi hii inahitaji ushirika wa pamoja kusaidiana na marafiki wa kweli katika maeneo ya kiroho na kijamii; kutoka katika mashirika mbalimbali duniani wenye mlengo moja wa kiimani na PAG Tanzania.<br>**Mpango Mkakati Ukurasa wa 125.** | Wafilipi 2:25.<br><br>Nehemia 7:70. |

| | | |
|---|---|---|
| **23/01/2024 JUMANNE** | **UCHUMBA, NDOA NA FAMILIA.**<br>- Boresha mahusiano ya ndoa na familia. Kanisa bora ni matokeo ya familia bora.<br>- Roho Mtakatifu akuwezeshe kushiriki semina na warsha za wanandoa katika siku ya wiki ya familia.<br>- Neema ya Mungu iwe juu ya familia zetu.<br>**Mpango Mkakati ukurasa wa 87.** | Ruthu 3:11.<br>Mithali 8:33.<br>1 Petro 3: 7. |
| **24/01/2024 JUMATANO** | **WATOTO NA VIJANA.**<br>- Wakurugenzi wa idara hizi wafanye kazi hii katika viwango bora vya juu ili tuwe na kizazi imara yenye viongozi bora katika kipindi kijacho.<br>- Tuwafundishe watoto wetu maadili mema itakayowafaa katika maisha.<br>- Vijana wetu wawe wanyenyekevu na utii maana fahari ya vijana ni nguvu zao.<br>**Mpango Mkakati ukurasa wa 96.** | Mithali 22:6.<br>Kumbukumbu 11:19.<br>Yoeli 2:28. |
| **25/01/2024 ALHAMISI** | **WANAUME NA WANAWAKE.**<br>- Uone umuhimu wa idara hizi mbili katika kulijenga kanisa lenye nguvu zaidi katika siku zijazo, ina mtandao mkubwa katika kanisa la mahali pamoja.<br>- Wakurugenzi wao kutoka ngazi zote wajitoe kikamilifu ili kuleta matokeo chanya kwa kanisa zima.<br>- Hamasika kujitoa katika kuhudhuria mikutano yao na kutoa msaada wa hali na mali watakaohitaji. | Yoeli 2:28.<br>Waebrania 10:25. |

| | | |
|---|---|---|
| **26/01/2024 IJUMAA** | **UJAZO WA ROHO MTAKATIFU.**<br>- Kila jumapili tuwaombee watu ujazo wa Roho Mtakatifu na kunena kwa lugha.<br>- Jiandae na kupokea uamsho wa kipekee katika moyo wako.<br>- Karama za Roho zitende kazi kwa kila mwamini maana sisi ni mwili wa Yesu Kristo.<br>- Mungu amwage Roho Mtakatifu kwa makanisa yote hasa **Baraza la Makanisa ya Kipentekoste Tanzania (BMKT) au The Council of Pentecostal Churches of Tanzania (CPCT).** Tuwe na umoja wa kweli kujenga Mwili wa Kristo. | Matendo 1:8.<br><br>1 Wakorintho 12:4. |
| **27/01/2024 JUMAMOSI** | **SHUKRANI.**<br>- Mwabudu Mungu kwa kujibu maombi yako. Mshukuruni Mungu kwa maombi yote uliyoyaomba maana amekwisha kusikia na kutenda.<br>- Mshukuru kwa ajili uamsho katika kanisa la PAG Tanzania. Mshukuru Mungu kwa mipango yote na maono ya kanisa maana Mungu anakwenda kutenda Makubwa. | Zaburi 106:1.<br>2 Mambo ya Nyakati 20:21.<br><br>Isaya 12:4. |
| **28/01/2024 JUMAPILI** | **MSHUKURUNI BWANA KWA KUWA NI MWEMA; KWA MAANA FADHILI ZAKE NI ZA MILELE. MSHUKURUNI MUNGU WA MIUNGU; KWA MAANA FADHILI ZAKE NI ZA MILELE. MSHUKURUNI BWAWA WA MABWANA; KWA MAANA FADHILI ZAKE NI ZA MILELE. ZABURI 136:1-26** | |
| | | |

**ASANTE KWA KUSHIRIKI!**